



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

**UHUISHAJI WA LESENI ZA UUGUZI NA UKUNGA KWA MUHULA  
WA 2024-2027**

***Dodoma, 28 Agosti, 2024.***

Ofisi ya Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, inapenda kuwataarifu wauguzi na wakunga ambao muda wa matumizi ya Leseni zao unaisha tarehe **31 Disemba 2024** kwamba, dirisha la kuhuisha leseni limfunguliwa tangu tarehe **01/07/2024** na litakuwa wazi hadi tarehe **31 Disemba, 2024** ambapo katika kipindi hicho, uhuishaji utafanyika kwa gharama za kawaida bila faini na ifikapo tarehe **01/01/2025** uhuishaji huo utaambatana na faini.

Kwa tangazo hili, kila Muuguzi na Mkunga unaelekezwa kuhuisha Leseni na kuhakikisha unakuwa na CPD points zinazohitajika, kama kigezo cha kuhuisha leseni yako inayokuruhusu kutoa huduma, sambamba na hilo, unakumbushwa kuingia kwenye mfumo wa Baraza <https://tnmcis.tnmc.go.tz/register> ili kukamilisha taratibu za kuhuisha leseni.

Aidha, mwongozo wa namna ya kujisajili na kuhuisha leseni unapatikana katika mfumo huo.

Ikumbukwe kuwa uhuishaji wa Leseni za uuguzi na ukunga ni suala la kisheria kama inavyoelekezwa katika **kifungu cha 21(2) na 38(1)** cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa kwa ajili ya kusimamia Wataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga ili kuulinda umma dhidi ya huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 na Kanuni zake.

Nawatakia utekelezaji mwema.

***Imetolewa na:***

Ndimmyake Mwakapiso  
**Mkuu wa Kitengo;**  
**Uhusiano na Mawasiliano**